JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UCHUKUZI
CHUO CHA TAIFA CHA USAFIRISHAJI

# FURSA YA MAFUNZO MAALUM YA MADEREVA WA MABASI YAENDAYO HARAKA (MWENDOKASI - BRT)

Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) kwa kushirikiana na Kampuni ya mabasi yaendayo haraka (UDART) kimeandaa mafunzo maalum ya madereva wa mabasi yaendayo haraka maarufu Mwendo Kasi (Bus Rapid Transit – BRT).

**Lengo la Mafunzo**
Kuwawezesha madereva wenye sifa stahiki kupata mafunzo ya kuwa madereva wa mabasi ya Mwendo Kasi (BRT). Mafunzo yatawawezesha washiriki kuendesha mabasi ya BRT kwa usalama na weledi kwa kufuata taratibu maalum za BRT, kutoa huduma bora kwa abiria, kutumia teknolojia za mfumo na kukabiliana na dharura kwa ufanisi.

**Mahali:** Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT), Mabibo Dar es Salaam.

**Muda wa Mafunzo:** Siku Sita (6)

**Tarehe ya kuanza:** 23-28 Februari , 2026

**Ada ya Mafunzo:** 150,000/=

**Sifa za Mwombaji**
Mwombaji anatakiwa kuwa na sifa zifuatazo
- Leseni Daraja *C Plain* iliyohakikiwa na Jeshi la Polisi,
- Cheti cha PSV kutoka Chuo kinachotambulika,
- Umri wa miaka 25 – 50,
- Uzoefu wa miaka mitatu (3).

Watakaofaulu katika mafunzo haya watapata fursa ya ajira katika mradi wa mabasi yaendayo haraka (BRT). Hata hivyo, vigezo na masharti ya ajira hizo yatazingatiwa.

www.nit.ac.tz rector@nit.ac.tz +255 222 213 701 nit_tanzania1 nit_tanzania